Hamjambo wanafunzi wa DPS! Mimi ni Anthony Green na ninasomea kwenye Ponitz Career Technology Center. Leo nitakusaidia kujifunza jinsi ya kutumia Greater Dayton Regional Transit Authority, pia inayojulikana kama RTA, kwa ajili ya usafiri wako wa shuleni. Kutoka hatua ya kupata njia, hadi kusafiri kwenye basi na kuwasili salama mahali unakoenda, video hii itaangazia kila kitu unachohitaji kujua ili kuanza kutumia RTA leo.

Hebu tuanze!

Kutafuta Njia
Kuna njia mbalimbali za kutafuta njia ya kukupeleka na kukutoa shuleni, au eneo jingine lolote.

Ikiwa unatumia simu yako, tafuta programu ya ramani za Google au Apple na uandike mahali unakoenda. Badilisha hali yako ya kusafiri hadi kutumia basi, hatua unayoweza kufanya kwa kugusa aikoni ya basi. Kutoka hapa, simu yako itaonyesha njia yako kutoka wakati wa kutembea hadi kwenye kituo cha mabasi, kusafiri kwenye basi, kutoka kwenye basi na kutembea hadi mahali pa mwisho unapoenda.

Mchakato huu unaweza kufanyika kwenye kompyuta ya mezani. Nenda tu kwenye ramani za Google, andika mahali unakoenda, badilisha hali ya usafiri kuwa basi na uangalie machaguo yako ya njia. Ikiwa eneo lako unaloanzia halijajazwa kwa sasa, unaweza kuandika katika anwani ya eneo utakaloanzia.

Pia unaweza kupakua programu ya Transit ya bila malipo ili uone njia. Andika eneo lako la sasa na mahali unakoenda ili uone njia ya RTA unayopaswa kufuata. Programu ya Transit pia itakuambia wakati unapaswa kuanza kutembea hadi kwenye kituoa cha mabasi ili kuwasili kabla ya basi kusimama.

Ingiwa ungependa kuona ratiba ya njia ya RTA kwa kina, unaweza kutembelea tovuti ya RTA kwenye iriderta.org. Kutoka hapo, teua njia na ubofye kila njia ili uone ramani, maeneo ya kusimama na nyakati za kuwasili.

Kusubiri kwenye Kituo cha Mabasi
Ni desturi bora kufika kwenye kituo chako cha mabasi angalau dakika 5 kabla ya wakati ambao basi limeratibiwa kuwasili. Unaposubiri kwenye basi, ni muhimu uwe mahali unapoonekana ili dereva wa basi ajue kuwa unasubiri. Njia bora ya kufanya hili ni kusimama na kupunga mkono unapoona basi likikaribia. Kumbuka kujiandaa na nauli, kwa kuwa na pasi yako mkononi kabla ya kuabiri basi.

Kuingia kwenye Basi na Kulipia Safari yako
Unapoingia kwenye basi, utahitaji kugusa pasi yako kwenye kisomaji cha malipo. Pasi ni nzuri kwa safari zisizo na kikomo katika kipindi cha siku 31. Kipindi cha siku 31 kinaanza mara ya kwanza unapogusa pasi yako. Ukipokea pasi mpya kabla ya ile ya zamani kuisha muda, usihuishe pasi mpya hadi uihitaji. Hatua hii itahakikisha kuwa unaendelea kuwa na safari zisizo

na kikomo mwezi ujao wote. Ni jukumu lako kukumbuka wakati ulihuisha pasi yako. Ili kufanya hili unaweza kunakili tarehe ya utambazaji wako wa kwanza na tarehe ya mwisho kwenye kadi.

PDS inawapa wanafunzi walio na pasi za kila mwezi. Pasi zitasambazwa kwenye kila shule ya upli kila mwezi. Tafadhali zungumza na mwalimu wako mkuu ikiwa unaihitaji. Fahamu kwamba kadi hizi hazitapakiwa tena na huisha muda baada ya siku 31.

Kusafiri kwenye Basi
Tafadhali kaa kwenye kiti, au simama na ushikilie papi za ngazi au kamba ya usalama basi linapoendeshwa. Ikiwa umesimama, tafadhali hakikisha kuwa uko nyuma ya mstari wa manjano mbele ya basi kwa usalama wako.

Sheria nyingine za barabarani ni pamoja na:

- Hakuna uvutaji sigara wa aina yoyote.
- Hakuna kula wala kunywa. Ukileta chakula au vinywaji garini, lazima viwe kwenye chombo kilichofungwa.
- Unaposikiliza muziki, vaa spika za masikioni.
- Epuka kuzungumza kwa simu.
- Wateja hawapaswi kutumia lugha chafu wala kushiriki katika tabia ya usumbufu.
- Uharibifu wa mali ya RTA hauruhusiwi.
- Lazima wateja wasafishe vitu kwenye njia baina ya viti ili kuwaruhusu wengine wapite.
- Ikiwa kuna viti vichache, tafadhali ruhusu wateja wakongwe na wale walio na ulemavu wakae karibu na mbele ya basi.

Tafadhali fuata sheria hizi na maagizo mengine yoyote uliyopewa na dereva. Sheria zisipofuatwa, abiria wanaweza kuondolewa kwenye basi.

Kutoka kwenye Basi
Wakati basi linakaribia kuwenye kituo chako, lazima umwambie dereva kuwa unahitaji kushuka kwa kuvuta kamba upande wa basi.

Vuta kamba *baada ya* kupita kituo chako *kabla* tu ya kile unachohitaji. Wakati unapotoka kwenye basi, tafadhali toka kupitia mlango wa nyuma ili kuwaruhusu watu wanaoingia kwenye basi watumie mlango wa mbele. Kumbuka kwamba trafiki haisimami kwa magari ya kubeba watu na mizigo – usiwahi kuvuka mbele ya basi na utiee sheria za barabarani na uangalie magari yanayokuja baada ya kutoka. Baada ya kutoka kwenye basi, unaweza kuendelea kutembea hadi eneo lako la mwisho. Tafadhali tahadhari unapovuka barabara na mikingamo.

Kujitayarishia Siku ya Kwanza ya Shule
Unaweza kujifunza kuabiri basi bila malipo wikendi, kwa kuwa RTA ina safari zisizolipishwa siku za Jumamosi na Jumapili hadi tarehe 4 Septemba. RTA itatoa ratiba mpya Jumapili, tarehe 14 Agosti. Hakikisha kuwa umeangalia ratiba hizo ili kujua nyakati sahihi za basi za siku yako ya kwanza ya shule. Ukiangalia ratiba kabla ya tarehe hiyo, nyakati hazitakuwa sahihi.

Ikiwa una maswali ya ziada kuhusu kutumia RTA, tafadhali tembelea iriderta.org.